**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MADABA**
**MTIHANI WA UTAMILIFU WA WILAYA 021 KISWAHILI**
**KIDATO CHA NNE**

---

Muda: Saa 3 18/06/**2021**

**MAELEKEZO:**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali kumi na mbili (12).
2. Jibu maswali yote katika sehemu A na B na maswali matatu (3) kutoka sehemu C
3. Zingatia maagizo ya kila sehemu na ya kila swali.
4. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa havitakiwi katika chumba cha mtihani.
5. Andika namba yako ya mtihani katika kila ukurasa wa karatasi utakayojibia.

**SEHEMU A, (Alama 15)**

***Jibu maswali yote katika sehemu hii.***

1. Chagua herufi ya jibu sahihi katika vipengele (i) hadi (x), kisha andika herufi ya jibu hilo katika karatasi yako ya kujibia.

(i) "Mtoto anacheza mpira polepole sana"

A. N+T+Sh+Ch
B. N+T+Sh+Sh+Ch
C. N+T+Ch+Sh
D. N+TS+T+Ch+Sh
E. Silabi, Neno, Kirai na Sentensi.N+T+Sh+Ch+Sh

(ii) Ni methali ipi kati ya hizi zifuatazo yenye maana sawa sawa na methali "Ndo!Ndo! Ndo! si chururu"

A. Pole pole ndio mwendo
B. Mwenda pole hajikwai
C. Simba mwenda pole ndio mla nyama
D. Haba na haba hujaza kibaba
E. Bandu bandu humaliza gogo

(iii)Mang'winda amekuwa mtoro sana. Neno lililopigiwa mstari limetumika kama aina gani ya neno?

A. Kitenzi kikuu
B. Kiunganishi
C. Nomino
D. Kitenzi kisaidizi

E. Kitenzi kishirikishi

(iv)Ni hali ya viambishi vya maneno ndani ya tungo kukubaliana na kushikamana ili kuleta maana iliyokusudiwa.

A. Tungo
B. Sentensi
C. Lugha
D. Upatanisho wa kisarufi
E. Lugha ya mazungumzo

(v) Ni upi mpangilio sahihi wa mjengo wa Tungo?

A. Kirai, Neno, Sentensi na Kishazi
B. Neno, Kirai, Kishazi na Sentensi
C. Kishazi, Kirai, Sentensi na Neno
D. Sentensi, Neno. Kishazi na Kirai

(vi)Bainisha tabia ya umbo lililopigiwa mstari katika kitezi ib-w-a

A. Kauli tendeka
B. kauli tendea
C. Kauli tendeana
D. Kauli tendwa
E. Kauli tendesha

(vii) Ipi ni fasili sahihi kuhusu "Vina "miongoni mwa fasili zifuatazo?

A. Mstari wa mwisho wa shairi unaobadilika ubeti mmoja hadi mwingine.
B. Mistari wa mwisho wa ubeti wa ushairi wenye kujirudia kutoka ubeti mmoja hadi mwingine.
C. Idadi ya silabi zinazopatikana katika mstari wa ubeti wa ushairi
D. Silabi za kati na mwisho za mstari wa ubeti wa shairi zenye mlio unaofanana.
E. Kifungu cha maneno kinachobeba wazo kuu mojawapo la ushairi

(viii) "Serikali imeweka mikakati kabambe ili kupunguza umaskini" Neno ili katika sentensi hii ni aina gani ya neon?

A. Kivumishi
B. Kiwakilishi
C. Kihisishi
D. Kielezi
E. Kiunganishi

(ix) ……………. Ni kipashio kidogo kabisa cha lugha chenye maana. Maana hiyo yaweza kuwa ya kisarufi au kileksika;

A. Isimu

B. Shina
C. Mzizi
D. Kiimbo
E. Mofimu

(x) Kiti cha mfalme kinaheshimiwa. Katika sentensi hii neno lililopigiwa msitari ni aina gani ya neno katika uainishaji wa maneno?

A. kiunganishi
B. Kihusishi
C. Kivumishi
D. Kiigizi
E. Nomino

| i | ii | iii | iv | v | vi | vii | viii | ix | x |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | |

To Get a full post, click here and then find a post in our Group as titled in this post!